TANGAZO LA SERIKALI NA. 888 la tarehe 15/12/2023

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ya mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ya mwaka 2023.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"daftari la wageni" maana yake ni kitabu maalumu kilichoandaliwa na mmiliki au kilichonunuliwa kwa lengo la kusajili na kutunza kumbukumbu za wageni wanaolala kwenye nyumba ya kulala wageni;

"gharama ya malazi" maana yake ni kiasi cha fedha kinachotozwa na mmiliki wa nyumba ya kulala wageni kwa mtu ambaye anapata huduma ya malazi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya